# Kitabu cha kabili cha Musa kikemigwa
# Kulawa
## Ulongozi

Kitabu cha Kulawa chogendeleza simulizi ya ulelo wa Abulahamu, isongile mkitabu cha Mwanduso. Iditwaga da Kulawa dofambula, “kusegela,” kinhu acho cholagusa iwanhu wa Izilaeli viwasegele mwiisi ya Misili na kubwela mwiisi ayo Imulungu iyalongile komgwaa Abulahamu. Iwanhu oifunza mbuli za Bibilia otogola kamba mbuli nyingi zili mkitabu cha Kulawa zandikigwa na mtula ndagu Musa, mbuli ayo yokoneka mkitabu chenyego. Kulawa 24:4 yolagusa Musa viyandike ikitabu kino. Ikifungu kili mna Yoshua 8:31 chotambula lagizo dili mna ikitabu cha Kulawa 20:25 na cholonga, “Kamba viyandikigwe mna ikitabu cha Malagizo ga Musa.” Mna idilagano da sambi dotambula miyanza mingi ivitabu vandikigwe na Musa, twahalola Maluko 12:26 yolonga kulawa “Ikitabu cha Musa” viilonga mbuli ya kija kilawililе mna ikisolo kikwaka. Ukusegela kwa iwanhu wa Izilaeli kulawa mwiisi ya Misili kulawila kamba miyaka 1300 hebu 1400 Kilisito yang'hali kuvumbuka. Mna ikitabu cha 1 Wandewa 6:1 yolonga kamba ukusegela kwa iwanhu wa Izilaeli kulawa mwiisi ya Misili kuvikiza miyaka 480 mna umwaka wa ikane wa kutawala Sulemani kamba mndewa wa iwanhu wa Izilaeli.

Kitabu cha Kulawa chogangamiza kwa

kulagusa vija Imulungu viyagavikize gaja gayamulongele Abulahamu na Isaka na Yakobo. Kitabu kino cholonga mbuli ng'hulu za Imulungu viyawakombole iwanhu wa ulelo wa Abulahamu, awo iwanhu wa Izilaeli, kulawa mwiisi ya Misili mwiisula ya 1 mbaka 12. Kulawa aho Imulungu kawalongoza wanhu zake kuna ulugongo lwa Sinai na ako kamgwaa Musa malagizo mengi ili Waizilaeli wagakweleleze mwiisula ya 12 mbaka 19. Malagizo gago gowalagusila viwolondigwa kukala na viwolondigwa kulava nhosa na wagweleligwa malagizo ga ukuzenga dihema da mting'hano, aho ihanhu honda yakale Imulungu hagati yao, na wagweleligwa malagizo ga ukutenda disanduku da lagano na ivinhu viyagwe vili mdihema ajo da kutambikila na iviwalo va ulava nhosa mwiisula ya 20 mbaka 31. Abaho vikulawile ukumulema Imulungu aho Waizilaeli viwatendile ikinyago cha zahabu cha ng'ombe, Musa kaiting'hana kabili na Imulungu mwiisula ya 32 mbaka 33. Kuuhelelo wa ikitabu, tosoma ivinhu vitambuligwe ako kukisogo vivitendigwe mwiisula ya 33 mbaka 40.

**Mbuli zili mkitabu**

Sula ya 1 yosimulila Waizilaeli viwakalile muutumwa ako mwiisi ya Misili.

Sula ya 2-4 zomtambula Musa na kulonga mbuli za ugima wake mbaka viyakemigwe yawakombole iwanhu wa Imulungu.

Abaho imwandikaji kolonga vija Imulungu viyatendile unzonza na mikubulo mwiisi ya Misili ili yawakombole wanhu zake kulawa mwiisi ayo na kulawa kwa iwakalizi wa Falao

(Sula ya 5-15).

Kulawa aho iwanhu wa Izilaeli wagendelela na umwanza na wavika kulugongo lwa Sinai (Sula ya 15-19).

Sula ya 20-31 tosoma vija Imulungu viyamgwelele Musa gamalagizo gakalile gamemile ivinhu viyalondile Imulungu ili wanhu zake, awo iwanhu wa Izilaeli, viwalondigwe kukala na kutambika.

Sula ya 32 yandika vija iwanhu wa Izilaeli viwamulemile Imulungu kwa kumsusumiza Haluni, ndugu yake Musa, yatende kinyago kiigalile na ng'ombe.

Sula ya 33-40 zolonga vija Musa viyonile ukulu wa Imulungu, na abaho kawafunza iwanhu wa Izilaeli malagizo ga Imulungu na va ukutenda dihema da mting'hano na disanduku da lagano na ivinhu viyagwe va ukutambikila mumo mdihema da mting'hano na iviwalo va ulava nhosa.

### *Waizilaeli odununzigwa mwiisi ya Misili*

1 Gano gago matwaga ga wana wa kimbigalo wa
Yakobo vivija kokemigwa Izilaeli wacholile Misili
hamoja na heyo, kila imoja na wanage,
2 Lubeni na Simeoni na Lawi na Yuda,
3 na Isakali na Zabuloni na Benjamini,
4 na Dani na Nafutali na Gadi na Asheli.
5 Ulelo wose wa Yakobo wakala wanhu malongo saba. Kipindi acho Yusufu kakala yalongole
mwaka kuko Misili.
6 Kumwande Yusufu kafa na ndugu zake na
wanhu wose wa ulelo uja wafa,

7 lakini Waizilaeli wengezeka ng'hani, wakala
na nguvu na wenela kila hanhu mwiisi ya Misili.
8 Abaho mndewa iyagwe katawala ako Misili,
mndewa ayo kakala hamjuwile bule Yusufu.
9 Kawalongela wanhu zake, “Loleni Waizilaeli
viweli wengi ng'hani na wana nguvu ng'hani
kubanza siye.
10 Avo kamba yahalawila ng'hondo, odaha
kuilumba na wanhu otwihila na kututowa, na
hewo olawanya mwiisi ino. Avo tuzahile nzila ya
kuwahunguza sikuwengezeke.”
11 Avo Wamisili weka wemilizi wawemilile
Waizilaeli na wawadununze kwa sang'hano
ndala. Waizilaeli wamzengela Falao mabuga ga
kwikila vinhu vake, mabuga gago gakala Pitomu
na Lamesesi.
12 Lakini viwagendelele kuwadununza,
vivo Waizilaeli viwagendelele kwengezeka na
kwenela mwiisi yose. Avo Wamisili wawadumba
ng'hani Waizilaeli.
13 Avo Wamisili wawatenda Waizilaeli kamba
watumwa kwa kuwagwaa sang'hano ndala.
14 Wautenda ugima wao uwe mdala kwa
kuwananahiza sang'hano ndala ya kuzenga
ng'anda na sang'hano zose za migunda. Waizilaeli
hawoneligwe bazi.
15 Avo mndewa wa Misili, kawalongela Shifila
na Pua iwang'hunga, waja owataza watwanzi wa
Kiebulania,
16 kawalongela, “Vonda muwataze watwanzi
wa kiebulania kipindi cha kulela, yahaleleka
mwana wa kitwanzi mulekeni lakini yahaleleka
mwana wa kimbigalo mkomeni.”

17 Lakini kwavija wang'hunga wao wakala om-
dumba Imulungu hawategeleze ziwalongeligwe
na mndewa wa Misili, wawaleka wana wa kimbi-
galo wawe wagima.
18 Avo mndewa wa Misili kawakema
wang'hunga awo kawauza, “Habali
hamuwakomile iwana wa kimbigalo?”
19 Hewo wamwidika, “Watwanzi wa Kiebula-
nia hawaigalile na watwanzi wa Kimisili, wat-
wanzi wa Kiebulania wana nguvu ng'hani, na
olela yang'hali mng'hunga hanavika.”
20 Avo Imulungu kawatendela ganogile awo
iwang'hunga, na Waizilaeli wengezeka na wakala
na nguvu ng'hani.
21 Kwavija awo iwang'hunga wakala omdumba
Imulungu, Imulungu kawatenda walele wana.
22 Abaho Falao kawalagiza wanhu zake wose,
kawalongela, “Kila mwana wa kimbigalo yonda
yavumbuke kwa Waebulania mwaseni muul-
wanda lwa Naili, lakini kamba mwana wa kit-
wanzi mulekeni mgima.”

# 2

*Kuvumbuka kwa Musa*
1 Kukala na munhu imoja wa kabila da Lawi,
yamsolile mtwanzi imoja, mtwanzi ayo vivija ko-
lawa mdikabila da Lawi.
2 Avo mtwanzi ayo kagoga inda, kalela mwana
wa kimbigalo. Viyamone mwana ayo kanoga
ng'hani, kamfisa kwa miyezi midatu.
3 Viyonile hadaha kumfisa kabili, kasola kisege
kilukigwe na milanzi kakibaka tongo tongo,
kamwika mwana ayo mkisege acho, abaho

kakizudika ikisege mmidete mgamazi kumgwazo
wa ulwanda lwa Naili.
4 Lumbu jake ija imwana, kaifisa behi ili yalole
choni chonda kimulawililile.
5 Avo mndele wa Falao kahumuluka
muulwanda yakoge, wasang'hanaji zake wa
kitwanzi wakala otembela tembela kumgwazo
wa ulwanda. Mndele wa Falao kachona kija
ikisege mmisanze, kamtuma msang'hanaji wake
yamgalile.
6 Mndele wa Falao viyakifungule ikisege acho
kamona mwana, kakala kolila. Heyo kamonela
bazi, kalonga, “Imwana ino vivija wa Waebula-
nia.”
7 Bahaja lumbu jake mwana ija kalawilila
kamuuza mndele wa Falao, “Kolonda nichole
kumkema mtwanzi wa Kiebulania yakong'hezele
mwana ino?”
8 Mndele wa Falao kamwidika, “Ona, genda
kamkeme.” Avo mndele ayo kachola kumkema
mamake imwana ayo.
9 Mndele wa Falao kamulongela mtwanzi
ayo, “Msole imwana ino unyong'hezele, na niye
nokuliha fungu jako.” Avo mtwanzi ayo kamsola
imwana na kumong'heza.
10 Mwana viyakalile mbala goya, kamgala kwa
mndele wa Falao, heyo kamsola na kamtenda
mwanage. Kalonga, “Kwavija nimvabula mga-
mazi,” avo kamkema Musa, fambulo jake kuvab-
ula.

### *Musa kokimbilila mwiisi ya Midiani*

11 Musa viyakulile, kachola kuwatembelela
ndugu zake Waebulania, kawona viwananahizwe

kusang'hana sang'hano ndala. Kamona
Mmisili imoja komtowa Muebulania, imoja wa
Waebulania wayage.
12 Musa kawegesela na viyone kuduhu munhu
yomulola, kamkoma Immisili na kamfisa
mmisanga.
13 Imitondo yake, Musa kachola kabili kawona
Waebulania wabili oitowa. Avo kamuuza ija
yomonela miyage, “Habali komtowa miyago?”
14 Munhu ayo kamwidika, “Nani yakwikile
uwe kilongozi wetu na msemi wetu? Kolonda
kunikoma kamba vuumkomile ija Immisili?”
Avo Musa kadumba na kailongela mwenyego,
“Kumbe wanhu oijuwa mbuli ino!”
15 Falao viyaihulike mbuli ayo ilawilile, kalonda
kumkoma Musa, lakini Musa kakimbila kachola
kukala mwiisi ya Midiani, kakala behi na sima.
16 Avo wandele saba wa mulava nhosa wa kuko
Midiani weza kudeha mazi ili wazing'weze fugo
za tatao.
17 Wasusilaji wayagwe weza wawawinga wan-
dele awo. Lakini Musa keza kawataza wandele
awo kwa kuzing'weza mazi fugo zao.
18 Viwabwelile kwa tatao Leueli, kawauza, “Ha-
bali lelo mulopola kubwela?”
19 Wao wamwidika, “Mmisili imoja katutaza
mmakono ga wasusilaji waja, heyo mwenyego
katudehela mazi na kuzing'weza fugo zetu.”
20 Tatao kawauza wandele zake, “Kakwahi? Ha-
bali mmuleka kuko? Mkemeni yeze yaje hamoja
na siye.”
21 Avo Musa katogola kukala kwa munhu ayo,
avo munhu ayo kamgwaa Musa mndele wake

yakemigwe Sipola yawe mwehe wake.
22 Sipola kamulelela Musa mwana wa kim-
bigalo. Musa kailongela mwenyego, “Niye sili
mwenekae mwiisi ino.” Avo kamgwaa twaga
mwana ayo Gelishomu, fambulo jake munhu
baki.

### *Waizilaeli oiyalala muutumwa*

23 Miyaka mingi viibitile mndewa wa Mis-
ili kafa, lakini Waizilaeli wagangamala na wa-
mulililila Imulungu kwavija wakala watumwa.
24 Imulungu kahulika kuiyalala kwao, na heyo
kakumbuka lagano jake diyatendile na Abula-
hamu na Isaka na Yakobo.
25 Imulungu kawalola Waizilaeli na kajuwa vi-
wodununzwa.

# 3

### *Imulungu komkema Musa*

1 Musa kakala kodisusila bumbila da
ng'hondolo wa tata mkwe wake Yetulo, imulava
nhosa wa ako Midiani. Musa kadigala bumbila
dijo mwambu wa kuluwala na kavika Holebu,
kulugongo lwa Imulungu.
2 Baho, msenga wa Mndewa Imulungu kamu-
lawililila Musa mna dilambi da moto ulawile hagati
ya ikisolo. Musa kachona ikisolo chokwaka moto
lakini hakilukula.
3 Musa kagelegeza, “Beta ng'hwese behi ndole
unzonza uno, habali kisolo chokwaka lakini hak-
ilukula.”
4 Mndewa Imulungu viyamonile kakwesa behi,
kamkema kulawa kuna ikisolo! “Musa! Musa!”
Musa kedika, “Niye nabaha.”

5 Imulungu kamulongela Musa, “Sikuukwese
behi! Vula vilatu vako kwavija aho hawimile
hong'ala.”
6 Abaho Imulungu kamulongela, “Niye na Imu-
lungu wa tatako, Imulungu wa Abulahamu na
Imulungu wa Isaka na Imulungu wa Yakobo.” Avo
Musa kagubika kihanga chake kwavija kadumba
kumulola Imulungu.

7 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela, “Nig-
ona madununzo gowopata wanhu zangu weli
kuko Misili. Mhulika viwoiyalala kwa kudunun-
zwa na waja owemilila. Kwavija nojuwa vi-
wogaya,
8 avo nihumuluka ili niwakombole walawe
mmakono gawa Misili na niwagale mwiisi
ng'hulu na inogile, isi imemile uki na maziwa, isi
ya Wakanaani na Wahiti na Waamoli na Wapelizi
na Wahivi na Wayebusi.
9 Na sambi kililo cha Waizilaeli kinivikila na
niwona Wamisili viwowadununza.
10 Sambi nokutuma kwa Falao, ili uwalave
wanhu zangu wa Izilaeli mwiisi ya Misili.”

11 Lakini Musa kamulongela Imulungu, “Niye
na nani mbaka nichole kwa Falao, nikawalave
Waizilaeli mwiisi ya Misili?”

12 Imulungu kamulongela, “Niye nokuwa
hamoja na gweye. Vonda uwalave wanhu wa
Izilaeli mwiisi ya Misili, monitambikila niye
kulugongo luno. Acho chokuwa kilagusa kamba
niye nikutuma.”

13 Musa kamulongela Imulungu, “Nahachola
kwa Waizilaeli kuwalongela, ‘Imulungu wa wa-

henga zenu kanhuma kumwenu,’ wao wahaniuza, ‘Twaga jake nani?’ Niwalongele choni?”

14 Imulungu kamulongela Musa, “Nene iyo Nene. Vino vivo viulondigwa kuwalongela Waizilaeli, ‘Ija yokemigwa Nene iyo Nene, kanhuma kumwenu.’ ”
15 Imulungu kamulongela Musa, “Walongele Waizilaeli kamba, ‘Niye Mndewa Imulungu, Imulungu wa wahenga zenu, Imulungu wa Abulahamu na Imulungu wa Isaka na Imulungu wa Yakobo nikutuma kumwao.’ Dino dijo twaga jangu milele, vino vivo ulelo wose vonda wanikumbuke.
16 Genda ukaiting'hane na wavele wa Izilaeli walongele kamba, ‘Niye Mndewa Imulungu, Imulungu wa wahenga zenu, Imulungu wa Abulahamu na Imulungu wa Isaka na Imulungu wa Yakobo, kandawila na kanilongela.’ Walongele, ‘Niwalola goya na nigona gaja gomutendeligwa mwiisi ya Misili.
17 Na niye nilonga kamba nowalava mwiisi ya Misili kuna gamagazo, nowagala mwiisi ya Wakanaani na Wahiti na Waamoli na Wapelizi na Wahivi na Wayebusi mwiisi imemile uki na maziwa.’

18 “Wao okutegeleza, abaho gweye na wavele wa Izilaeli mochola kwa mndewa wa Misili na kumulongela, ‘Mndewa Imulungu, Imulungu wa Waebulania katulawila siye. Avo tutogolele tuchole kwa siku ndatu kuluwala tukamulavile nhosa Mndewa Imulungu wetu.’
19 Nojuwa mndewa wa Misili honda yawatogolele muchole mbaka yananahizwe kwa nguvu.

20 Lakini nougolosa mkono wangu na
kuwakoboza Wamisili kwa vilaguso vonda
nitende kuko. Abaho Falao kowaleka musegele.
21 “Abaho nowatenda Wamisili wawatendele
ganogile Waizilaeli ili vonda musegele mwiisi ya
Misili, sikumusegele makono gaiyeka.
22 Kila mtwanzi wa Kiebulania yampule Mmisili
yokala behi na heyo hebu mgeni yokala mng'anda
yake viwalo na vinhu va kuihamba va zahabu na
shaba. Avo mowavaza wanenu wa kitwanzi na
wa kimbigalo vinhu avo vose. Vino vivo vonda
musole vinhu va Wamisili.”

# 4

*Imulungu komgwaa Musa udahi wa kutenda unzonza*

1 Abaho Musa kamulongela Mndewa Imulungu,
“Avo yokuwaze kamba Waizilaeli hawanhogola
na hawanitegeleza vonda niwalongele. Onon-
gela, ‘Mndewa hakulawile bule’?”
2 Avo Mndewa Imulungu kamuuza, “Kugoga
choni mmakono?”
Kamwidika “Fimbo.”
3 Mndewa kamulongela, “Ibwanhe hasi.” Musa
viyaibwanhe hasi, igaluka mgendela hasi, Musa
kakimbila.
4 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela Musa,
“Golosa mkono wako mgoge umkila.” Avo Musa
kagolosa mkono wake kamgoga umkila, na im-
gendela hasi kagaluka fimbo kabili.
5 Mndewa Imulungu kamulongela, “Utende
vino ili Waizilaeli watogole kamba niye Mndewa,

Imulungu wa wahenga zao, Imulungu wa Abu-
lahamu na Imulungu wa Isaka na Imulungu wa
Yakobo nikulawila."
6 Mndewa Imulungu kamulongela kabili Musa,
"Ingiza mkono wako mna ikiwalo chako." Avo
Musa kengiza mkono wake mna ikiwalo chake
na viyaulavile kunze, ukala na utamu wa dikulu
ukala mzelu kamba pamba.
7 Abaho Imulungu kamulongela, "Ingiza
kabili mkono wako mna ikiwalo chako!" Musa
kawingiza mkono wake mna ikiwalo chake,
viyaulavile kunze mkono wake ubwela kamba
viwili lukuli lwake.
8 Imulungu kamulongela Musa, "Kamba oleka
kukutogola kwa unzonza wa ichanduso, odaha
kutogola kwa unzonza wa kabili.
9 Lakini kamba hawakutogole kwa vinhu avo vi-
bili, wahalema kukutegeleza kwa gaja gaulongile,
deha mazi ga lwanda lwa Naili ugete mwiisi. Mazi
gago gogaluka damu."
10 Musa kamulongela Mndewa Imulungu, "Aka
Mndewa sikuunhume niye. Niye sidahile bule
kulonga goya toka mwaka, hata sambi viusongile
kulonga na niye msang'hanaji wako. Niye sili
mulongaji."
11 Mndewa Imulungu kamuuza, "Nani
yalumbile mulomo wa munhu? Nani yomtenda
munhu sikuyalonge hebu mvugu? Yalole hebu
msuwameso? Vino sili niye Mndewa Imulungu?
12 Avo, genda! Nokutaza kulonga, nokufunza
cha kulonga."
13 Lakini Musa kamwidika, "Mndewa wangu,
chonde mtume munhu iyagwe."

14 Mndewa Imulungu kamgevuzikila Musa, ka-
mulongela, “Gweye sikunayo ndugu yako Haluni
ija Imulawi? Nojuwa heyo kodaha kulonga
vinogile. Sambi kamnzila kokwiza kuiting'hana
na gweye na yahakona kodeng'helela.
15 Gweye longa nayo na mulongele gaja gonda
yalonge. Niye nowataza, na kuwafunza ga uku-
sang'hana.
16 Haluni kolonga na Waizilaeli hanhu hako.
Heyo kokuwa mulongaji wako na gweye kokuwa
kamba Imulungu kumwake.
17 Sola ifimbo ino ili mmakono gako, avo koitu-
mia kutenda unzonza.”

### *Musa kobwela Misili*

18 Abaho Musa kabwela kwa Yetulo, tata mkwe
yake, kamulongela, “Chonde nokupula nhogolela
nibwele Misili kwa ndugu zangu, nikawakagule
kamba wang'hali wagima.” Yetulo kamulongela,
“Genda moyo uholile.”
19 Musa viyakalile yang'hali mwiisi ya Midiani,
Mndewa Imulungu kamulongela, “Bwela Misili
kwavija waja wose walondile kukukoma wafa.”
20 Avo Musa kamsola mwehe wake na wanage,
kawakweza mumgongo wa kihongwe, kasonga
mwanza wa kubwela Misili, Musa kasola fimbo
iyalongeligwe na Imulungu yaisole.
21 Mndewa Imulungu kamulongela Musa, “Wa-
havika mwiisi ya Misili sang'hana mgameso ga
Falao unzonza wose unikugwelele udahi wa ku-
sang'hana. Lakini noutenda moyo wa Falao uwe
mdala avo honda yawaleke Waizilaeli wasegele.

22 Abaho gweye komulongela Falao, Mndewa
Imulungu kalonga vino, ‘Wanhu wa Izilaeli
kamba mwanangu chaudele wa kimbigalo.
23 Na niye nokulongela muleke mwanangu
yasegele, ili yakanitambikile, lakini humulekesa
bule yasegele, avo nomkoma chaudele wako wa
kimbigalo.’ ”

24 Viyakalile yang'hali mnzila kobwela Misili,
Musa kakala mng'anda ya kuwasa wageni, Mn-
dewa Imulungu kamcholela kalonda kumkoma.
25 Lakini Sipola mwehe wake Musa kasola
dibwe dikutwa, kadikanha govi da mwanage,
kamkwasa najo mmagulu gake, kalonga, “Gweye
kwa mkasano wa damu kumwangu.”
26 Avo Mndewa Imulungu kamuleka Musa yawe
mgima, kwavija Sipola viyamwingize kumbi
kakala yalongile, “Mkasano wa damu.”

27 Mndewa Imulungu kamulongela Haluni,
“Chola kuluwala ukaiting'hane na Musa.” Avo
Haluni kachola kuiting'hana na Musa kulugongo
lwa Imulungu, viyamone kamnonela.
28 Abaho Musa kamulongela Haluni gaja gose
gayalongeligwe na Mndewa Imulungu viyamu-
longele yabwele Misili, vivija kamulongela un-
zonza wose uyalongeligwe yasang'hane.
29 Avo Musa na Haluni wachola Misili,
wawakema wavele wose wa Izilaeli.
30 Haluni kawalongela gose Mndewa Imulungu
gayamulagize Musa na vivija Musa katenda un-
zonza mgameso ga wanhu wose.
31 Wanhu watogola, na viwahulike kamba Mn-
dewa kawezila na kagona madununzo gao na

kolonda kuwataza, waidulika wamtambikila Mndewa Imulungu.

# 5

### *Musa na Haluni ochola kwa Falao*

1 Abaho Musa na Haluni wachola kwa Falao
wamulongela, “Mndewa Imulungu, Imulungu
wa Izilaeli kolonga vino, ‘Waleke wanhu zangu
wasegele, wakanitendele nyimwilinyimwili kuluwala.’ ”
2 Lakini Falao kawauza, “Mndewa Imulungu
ayo nani mbaka nimtegeleze na niwaleke
Waizilaeli wasegele? Niye simjuwile bule ayo
Mndewa Imulungu, na siwaleka Waizilaeli
wasegele.”
3 Musa na Haluni wamwidika, “Imulungu wa
Waebulania katulawila siye. Tuleke tuchole kuluwala kwa mwanza wa siku ndatu tukamulavile nhosa Mndewa Imulungu wetu. Wahalema
sikutusegele Mndewa Imulungu kotukoma kwa
mitamu hebu kwa ng'hondo.”
4 Mndewa wa Misili kawedika, “Gweye Musa na
miyago Haluni habali mowatenda wanhu waleke
kusang'hana? Bweleni mzisang'hano zenu.”
5 Abaho Falao kalonga kabili, “Wanhu wenu
wengi kubanza wanhu wa isi yangu, na sambi
mweye molonda waleke kusang'hana!”
6 Siku didija Falao kawalagiza Wamisili iwakulu
wa watumwa hamoja na iwemilizi owemililaga
Waizilaeli wayao, kalonga,
7 “Sikumuwagwelele Waizilaeli minyomvi ya
kutendela matofali, walekeni wenyego wachole
kuizahila.

8 Lakini wingi wa matofali gondawatende uwe
uuja kamba wa siku zose, na sikudiswele hata
tofali dimoja, kwavija wanhu wano wanyeka,
lekaavo onongela, 'Tuleke tuchole tukamulavile
nhosa Imulungu wetu.'
9 Wengezeni wanhu wano sang'hano ndala
zonda ziwatende sikuwategeleze mbuli za uvizi."

10 Avo Wamisili iwakulu wa watumwa hamoja
na iwemilizi owemililaga Waizilaeli wayao wa-
chola kwa iwanhu kuwalongela, "Falao kalonga
vino, 'Siwagwelela kabili minyomvi.
11 Gendeni mweye wenyego kokose kumudaha
kuipata, lakini wingi wa matofali uwe vivija
kamba siku zose.' "
12 Avo wanhu wapwililika kila hanhu mwiisi ya
Misili kuzahila minyomvi.
13 Nao Wamisili iwakulu wa watumwa, wawala-
giza wanhu walonga, "Tendeni matofali kamba
gaja gamukalile motenda siku zose vimukalile
mogaliligwa minyomvi."
14 Wamisili iwakulu wa watumwa wawatowa
iwemilizi owemililaga Waizilaeli wayao, wasag-
uligwe kwimililila sang'hano kuno owalongela,
"Habali hamuvikize wingi wa matofali gagaja
kamba vimutendaga siku zose?"

15 Abaho iwemilizi owemililaga Waizilaeli
wayao wachola kwa Falao, wamulongela,
"Go, mkulu habali kotutendela vino siye
wasang'hanaji zako?
16 Hatugweleligwa kabili minyomvi na kuno
tolongeligwa tutende matofali. Abaho totoigwa
lakini wabanange wanhu zako mwenyego."

17 Falao kawedika, “Mweye mnyeka, na hamu-
londa kusang'hana, lekaavo monongela, ‘Tuleke
tuchole tukamulavile nhosa Mndewa Imulungu.’
18 Bweleni kusang'hana! Honda mugweleligwe
minyomvi, lakini molondigwa mutende matofali
kamba gaja gamutendaga siku zose.”
19 Avo iwemilizi owemililaga Waizilaeli wayao
wayona wa mmagazo ng'hani kwavija walon-
geligwa, “Mutende matofali kamba gaja gamu-
tendaga siku zose.”
20 Viwasegele kwa Falao, wamting'hana Musa
na Haluni wakala owabeta.
21 Avo wawalongela, “Mndewa Imulungu
yakilole kija kimutenda na yawataguse mweye
kwavija mumtenda Falao na wasang'hanaji
zake watwihile. Mweye muwagwelela mbuli
ya kutukomela.”

*Musa komuyalalila Mndewa Imulungu*

22 Abaho Musa kachola kwa Mndewa Imulungu
kabili kamulongela, “Mndewa Imulungu habali
kowatendela gehile wanhu wano? Avo kumbe
kino acho kiunitumile?
23 Toka vinicholile na kulonga na Falao kwa
twaga jako, mndewa ayo kowatendela gehile
wanhu wano, na gweye hutendile kinhu chochose
kuwakombola wanhu zako.”

# 6

1 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela Musa,
“Sambi kochona chonda nimtendele Falao. Kwa
udahi wangu kowaleka wanhu zangu wasegele.
Nayo kowawinga wasegele mwiisi yake kwa
udahi wangu.”

## *Imulungu kolonga kowakombola Waizilaeli*

2 Imulungu kamulongela Musa, “Niye na Mn-
dewa Imulungu.
3 Nimulawililа Abulahamu na Isaka na Yakobo,
njuwika kamba Imulungu yeli na Udahi wose,
lakini siwalongele bule kamba twaga jangu Mn-
dewa Imulungu.
4 Vivija niilagana nao kuwagwaa isi ya Kanaani,
kuko kuwakalile kamba wanhu baki.
5 Sambi nihulika kuiyalala kwa Waizilaeli vi-
wodununzwa na Wamisili, avo nidikumbuka
lagano jangu.
6 Walongele Waizilaeli vino, ‘Niye Mndewa
Imulungu, nowalava mwiisi ya Misili. Nowatenda
mulekeswe kulawa muutumwa. Nougolosa
mkono wangu na nowakoboza Wamisili na
kuwakombola mweye.
7 Nowatenda muwe wanhu zangu, na niye
nokuwa Imulungu wenu. Mojuwa kamba niye
na Mndewa Imulungu, Imulungu wenu, vonda
niwalave muutumwa ako Misili.
8 Nowagala mwiisi ija inilongile kwa kuiduwila
nowagwaa Abulahamu na Isaka na Yakobo.
Nowagwaa mweye isi ayo iwe yenu. Niye na
Mndewa Imulungu.’ ”
9 Musa kawalongela Waizilaeli mbuli azo, lakini
hewo hawamtegeleze bule, kwavija wakala na
lusikisiki mmizoyo yao mbuli ya magazo ga
utumwa.
10 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela
Musa,
11 “Genda kamulongele Falao, mndewa wa Mis-
ili, yawaleke Waizilaeli wasegele mwiisi yake.”

12 Lakini Musa kamwidika Mndewa Imulungu,
"Kamba Waizilaeli hawanitegeleze, avo Falao
konitegeleza vilihi? Na niye munhu mwenyego
sili mulongaji."
13 Lakini Mndewa Imulungu kalonga na Musa
na Haluni na kawalagiza wachole kwa Falao, mndewa wa Misili, wawalave Waizilaeli mwiisi ya
Misili.

### *Matwaga gayagwe ga iwahenga wakulu wa Waizilaeli*

14 Gano gago matwaga ga iwahenga wakulu wa
Waizilaeli.

Wanage Lubeni chaudele wa Izilaeli wakala,
Hanoki na Palu na Hesiloni na Kalimi. Wano
wakala wahenga wa kabila da Lubeni.
15 Wanage Simeoni wakala, Yemueli na
Yamini na Ohadi na Yakini na Sohali na Shauli
yakalile mwana wa mtwanzi wa Kanaani.
Wano wakala wahenga wa kabila da Simeoni.
16 Gano gago matwaga ga wana wa kimbigalo
wa Lawi, Gelishoni na Kohati na Melali. Lawi
kawa mgima kwa miyaka gana na malongo madatu na saba.
17 Wanage Gelishoni wakala, iwakulu wa
lukolo lwa Libini na Shimei.
18 Wanage Kohati wakala, Amulamu na Ishali
na Hebuloni na Uzieli. Kohati kawa mgima kwa
miyaka gana malongo madatu na ndatu.
19 Wanage Melali wakala, Mahili na Mushi.
Wano awo iwahenga wa kabila da Lawi.

20 Amulamu kamsola Yokebedi lumbu wa
tatake, nayo kamulela Musa na Haluni. Amulamu

kawa mgima kwa miyaka gana dimoja na malongo madatu na saba.

21 Wanage Ishali wakala, Kola na Nefegi na Zikili.
22 Wanage Uzieli wakala, Mishaeli na Elisafani na Sitili.
23 Haluni kamsola Elisheba, mndele wa Aminadabu na lumbu jake Nashoni, nayo kamulelela Nadabu na Abihu na Eleazali na Itamali.
24 Wanage Kola wakala, Asili na Elikana na Abiasafu, wano wakala wahenga wa lukolo lwa Kola.
25 Eleazali mwanage Haluni kamsola mndele wa Putieli, nayo kamulelela Finehasi.

Wano awo iwahenga wakulu wa kabila da Lawi.

26 Musa na Haluni awo walongeligwe na Mndewa Imulungu, “Muwalave Waizilaeli mwiisi ya Misili kwa ng'holo zao.”
27 Ona awo wamulongele Falao, mndewa wa Misili, yawaleke Waizilaeli wasegele.

### *Mndewa Imulungu kowalagiza Musa na Haluni*

28 Kipindi acho Mndewa Imulungu viyalongile na Musa mwiisi ya Misili,
29 kamulongela, “Niye na Mndewa Imulungu. Mulongele Falao, mndewa wa Misili, gaja gose gonikulongela.”
30 Lakini Musa kamwidika Mndewa Imulungu, “Niye sili mulongaji, avo Falao konitegeleza vilihi?”

# 7

1 Avo Mndewa Imulungu kamulongela Musa,
“Nokutenda gweye kamba Imulungu kwa Falao,
na ndugu yako Haluni kokuwa kamba mtula
ndagu wako.
2 Mulongele ndugu yako Haluni gaja gose
gonda nikulagize, nayo Haluni komulongela
Falao yawaleke Waizilaeli wasegele mwiisi yake.
3 Lakini noutenda moyo wa Falao uwe mdala.
Hata nahakongeza unzonza na vilaguso mwiisi ya
Misili,
4 Falao hakutegeleza bule. Abaho nougolosa
mkono wangu uli na udahi na kuwakoboza
Wamisili na nozilava ng'holo za Waizilaeli.”
5 Na Wamisili ojuwa kamba niye na Mndewa
Imulungu vonda niugolose mkono wangu
kumwao na kuwalava Waizilaeli mwiisi yao.
6 Musa na Haluni wasang'hana kamba viwalag-
izwe na Mndewa Imulungu.
7 Kipindi viwalongile na Falao, Musa kakala
na miyaka malongo nane na Haluni kakala na
miyaka malongo nane na ndatu.

### *Fimbo ya Haluni*

8 Mndewa Imulungu kamulongela Musa na
Haluni,
9 “Mndewa wa Misili yahawalongela, ‘Tendeni
unzonza,’ mulongele Haluni yasole fimbo yake
yaibwanhe hasi mgameso ga Falao, nayo yo-
galuka mgendela hasi.”
10 Avo Musa na Haluni wachola kwa Falao
na watenda kamba viwalagizwe na Mndewa
Imulungu. Haluni kaibwanha hasi fimbo yake

mgameso ga Falao na watawala wake, nayo
igaluka mgendela hasi.
11 Abaho Falao kawakema wanhu wake weli na
nzewele na wahawi wake, na kwa uhawi wao
watenda vivija.
12 Kila imoja wao kaibwanha hasi fimbo yake,
na fimbo zao zigaluka mgendela hasi. Lakini
fimbo ya Haluni igaluke mgendela hasi izimeza
fimbo zao zigaluke mgendela hasi.
13 Hata avo zoyo da Falao dikala dala na hawa-
tegeleze bule Musa na Haluni, kamba Mndewa
Imulungu viyalongile.

### *Mazi ga lwanda lwa Naili gogaluka damu*

14 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela
Musa, "Moyo wa Falao mdala na kolema
kuwaleka Waizilaeli wasegele.
15 Avo uidamuke ulukwili ukaiting'hane na
Falao viyochola kuulwanda lwa Naili. Isole fimbo
ija igaluke mgendela hasi, umbete kumgwazo wa
lwanda.
16 Abaho umulongele vino, 'Mndewa Imulungu,
Imulungu wa Waebulania, kanhuma kumwako
nikulongele uwaleke wanhu zake wasegele, wa-
chole wakamtambikile kuluwala, lakini mbaka
sambi gweye hutegeleza.
17 Avo Mndewa Imulungu kolonga vino, sambi
komjuwa heyo iyo nani. Nogatowa mazi ga
lwanda lwa Naili kwa fimbo ino, na mazi gose
gogaluka damu.
18 Somba weli muulwanda lwa Naili wofa,
lwanda lonung'ha bundo, na Wamisili honda
walonde kugang'wa mazi gake.' "

19 Mndewa Imulungu kamulongela Musa, “Mu-
longele Haluni yasole fimbo yake na yaigolose
uchanha ya mazi gose ga Misili, mvizanda vose
mna imifuluta mna ivikolongo vose na mna
gamalamba, vose avo vogaluka damu. Damu
yokuwa kila hanhu mwiisi yose hata mna iviya va
mibiki na mabwe.”
20 Musa na Haluni watenda kamba Mndewa
Imulungu viyawalagize. Haluni kenula fimbo
yake mgameso ga Falao na watawala zake ka-
gatowa mazi ga lwanda lwa Naili, na mazi gose
gagaluka damu.
21 Somba wakalile muulwanda lwa Naili wafa.
Mazi gake ganung'ha bundo mbaka Wamisili
hawadahile kugang'wa mazi gake. Damu ikala
kila hanhu mwiisi ya Misili.
22 Lakini wahawi wa Misili kwa uhawi wao wa-
tenda kamba vivo. Avo zoyo da Falao digendelela
kuwa dala, na heyo hawategeleze Musa na Haluni
kamba viyalongile Mndewa Imulungu.
23 Avo, Falao kabwela ukae kumwake, na ha-
gagelegeze gaja galawilile.
24 Wamisili wose wakala ohimba kumgwazo wa
lwanda lwa Naili wapate mazi ga kung'wa, kwav-
ija hawadahile kung'wa mazi ga lwanda lulo.
25 Zibita siku saba toka Mndewa Imulungu viya-
gagaluse mazi ga lwanda.

# 8

*Mibula*

1 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela Musa,
“Chola kwa Falao mulongele Imulungu kolonga,

‘Waleke wanhu zangu wasegele, wakanitambikile.
2 Wahalema, noibananga isi yako kwa kugala mibula.
3 Lwanda lwa Naili lomema mibula na mibula ayo yokwingila mng'anda yako na mdigati jako na mulusazi lwako luuwasa, na mzing'anda za watawala zako na mzing'anda za wanhu zako hata mna iviya venu va kutelekela.
4 Mibula ayo yokwela mulukuli lwako, na mna izing'huli za wanhu zako na watawala zako.’ ”

5 Mndewa Imulungu kamulongela Musa, “Mulongele Haluni yenule fimbo yake uchanha ya vizanda na imifuluta na vikolongo, na mibula yolawilila na kuigubika isi yose ya Misili.”
6 Avo Haluni kenula fimbo yake uchanha ya mazi gose ga Misili, na mibula ilawilila na kuigubika isi yose ya Misili.
7 Lakini wahawi wa Misili watenda kamba vivo kwa uhawi wao, na vivija watenda mibula ilawilile mwiisi ya Misili.

8 Abaho Falao kawakema Musa na Haluni kawalongela, “Mpuleni Mndewa Imulungu yaisegese mibula ino kumwangu na kwa wanhu zangu, na niye nowaleka wanhu zenu wachole kumulavila nhosa Mndewa Imulungu.”

9 Musa kamwidika Falao, “Sagula gweye lini kolonda nikupulile gweye hamoja na watawala zako na wanhu zako mibula isegele mzing'anda zenu na wasigale muulwanda wiiyeka.”

10 Falao kalonga, “Nipulile mayo.”

Musa kamwidika, “Notenda kamba viulongile ili ujuwe kuduhu yoyose yaigalile na Mndewa

Imulungu, Imulungu wetu.
11 Mibula ayo yosegela kumwako na
mzing'anda zenu na watawala wako na kwa
wanhu zako, mibula ayo yosigala muulwanda
wiiyeka.”
12 Abaho Musa na Haluni wasegela kwa Falao,
Musa kampula Mndewa Imulungu, yaisegese
mibula ikalile kwa Falao.
13 Mndewa Imulungu katenda kamba Musa
viyampulile. Mibula ikalile mzing'anda na mna
gamabuga na mmigunda ifa.
14 Wanhu waika hamoja mibula yose ifile, na isi
yose inung'ha bundo.
15 Lakini Falao viyonile mibula ifa, zoyo jake
dikala dala kabili, hawategeleze Musa na Haluni
kamba Mndewa Imulungu viyalongile.

*Mhani*

16 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela
Musa, “Mulongele Haluni, yenule fimbo yake
yatoe timbwisi da isi, najo dogaluka mhani mwiisi
yose ya Misili.”
17 Avo Haluni viyenule fimbo yake na kuitowa
hasi, timbwisi digaluka mhani wawananahila
wanhu na wanyama. Timbwisi jose da isi ya Misili
digaluka mhani.
18 Wahawi wa Misili kwa uhawi wao wageza
kugalusa timbwisi diwe mhani lakini hawadahile
bule. Mhani wakala wenele kwa wanhu na
wanyama.
19 Wahawi wamulongela Falao, “Uno mkono
wa Imulungu!” Lakini zoyo da Falao digendelela
kuwa dala na halondile kuwategeleza Musa na
Haluni kamba Mndewa Imulungu viyalongile.

### *Mikonzi*

20 Mndewa Imulungu kamulongela Musa,
“Uidamuke ulukwili ukaiting'hane na Falao
viyochola kuulwanda. Mulongele kamba
Mndewa Imulungu kolonga, ‘Waleke wanhu
zangu wasegele, wakanitambikile.
21 Wahalema kuwaleka wasegele, nogala
mikonzi kumwako gweye na watawala zako na
kwa wanhu zako wose. Ng'anda za Wamisili
zomema mikonzi na vivija isi yose yomema
mikonzi.
22 Lakini mdisiku dijo kuna umwambu wa
Gosheni, kuko kowokala wanhu zangu kokuwa
kuduhu mikonzi, ili ujuwe kamba niye Mndewa
Imulungu nosang'hana mwiisi ino.
23 Nowabagula wanhu wako na wanhu wangu,
unzonza uno noutenda mayo.’ ”
24 Avo Mndewa Imulungu katenda kamba viya-
longile, kagala madali ga mikonzi ingile mng'anda
ya Falao na mna zing'anda za watawala zake. Isi
yose ya Misili inangigwa na mikonzi ayo.

25 Abaho Falao kamkema Musa na Haluni kawa-
longela, “Gendeni mkamulavile nhosa Imulungu
wenu mmuno mwiisi ya Misili.”

26 Musa kamwidika, “Aka havinogile bule ku-
tenda vivo, kwavija nhosa zonda tumulavile Mn-
dewa Imulungu wetu zowagevuza Wamisili. Avo
twahalava nhosa ziwagevuza okwiza kutukoma
kwa mabwe.
27 Tolondigwa tugende mwanza wa siku ndatu
kuluwala, tukamulavile nhosa Mndewa Imu-
lungu wetu, kamba viyatulagize.”

28 Falao kalonga, “Nowaleka musegele muc-
hole mkamulavile nhosa kuluwala Mndewa Imu-
lungu, Imulungu wenu, lakini sikumuchole kutali
ng'hani. Mhulileni na niye.”
29 Musa kamwidika Falao, “Nahasegela hano
nompula Imulungu, mayo mikonzi ino yosege-
sigwa kumwako gweye, na kwa watawala wako
na kwa wanhu zako. Lakini sikuutuvizile kabili
na kuwagomesa wanhu sikuwachole kumulavila
nhosa Mndewa Imulungu.”
30 Abaho Musa kasegela kwa Falao, na kampula
Mndewa Imulungu.
31 Mndewa Imulungu katenda vivija kamba
Musa viyapulile. Mikonzi isegela kwa Falao, na
kwa watawala zake na kwa wanhu zake, kuduhu
hata ng'honzi imoja yasigale.
32 Lakini hata mwanza uno zoyo da Falao dikala
dala na hawalekile Waizilaeli wasegele.

# 9

### *Kufa kwa wanyama*

1 Abaho Mndewa kamulongela Musa, “Genda
kwa Falao mulongele, Mndewa Imulungu, Imu-
lungu wa Waebulania, kolonga, ‘Waleke wanhu
zangu wasegele, wakanitambikile.
2 Wahalema kuwaleka wasegele,
3 nougolosa mkono wangu na kugala mitamu
mzifugo zako zose, ng'ombe na falasi na vihongwe
na ngamiya na mbuzi na ng'hondolo.
4 Lakini Mndewa Imulungu kobagula fugo za
Waizilaeli na fugo za Wamisili, avo mzifugo za
Waizilaeli kokuwa kuduhu hata mnyama imoja
yonda yafe.’ ”

5 Mndewa Imulungu keka siku kalonga, “Mayo
Mndewa kotenda mbuli ino mwiisi ino.”
6 Imitondo yake Mndewa Imulungu katenda
kamba viyalongile, na fugo zose za Misili zifa,
kuduhu hata mnyama imoja wa Waizilaeli yafile.
7 Falao kawatuma wanhu wakauze mbuli ya
fugo za Waizilaeli, wamulongela kuduhu hata
mnyama imoja wa Waizilaeli yafile. Lakini zoyo
da Falao digendelela kuwa dala na halondile
kuwaleka wasegele.

### *Mipute*

8 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela Musa
na Haluni, “Kila imoja yadehe mitozi ya tanuli
ganza dimoja, abaho Musa yaipwililise uchanha
mgameso ga Falao
9 Mitozi ayo yokuwa timbwisi na dopwililika
mwiisi yose ya Misili. Timbwisi dijo dogala
mipute na yahatumbuka yokuwa milonda kwa
wanhu na wanyama mwiisi yose ya Misili.”
10 Avo wadeha mitozi kulawa mditanuli wa-
chola kwa Falao, na Musa kaipwililisa uchanha
mgameso ga Falao. Wanhu na wanyama wapata
mipute na viitumbuke iwa milonda.
11 Iwahawi hawadahile kwima kuulongozi wa
Musa mbuli ya mipute ikalile kumwao na ikalile
kwa Wamisili wose.
12 Lakini Mndewa Imulungu kamtenda Falao
yawe na moyo mdala na hawategeleze, kamba
Mndewa Imulungu viyamulongele Musa.

### *Mvula ya mabwe*

13 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela
Musa, “Lamuka imitondo ng'hani uchole kwa

Falao. Mulongele kamba Mndewa Imulungu, Imulungu wa Waebulania kolonga, ‘Waleke wanhu zangu wasegele, wakanitambikile.

14 Kwavija mwanza uno nokukoboza gweye na watawala zako na wanhu zako, baho kojuwa kamba kuduhu iyagwe mwiisi yose yaigalile na niye.

15 Kwavija mbaka sambi nahagolose mkono wangu na kukutowa gweye na wanhu zako na mwahafile mwaka.

16 Lakini niwaleka muwe wagima kulagusa udahi wangu avo wanhu wose wa mwiisi wadijuwe twaga jangu.

17 Lakini zoyo jako ding'hali dala na hulonda kuwaleka wanhu zangu wasegele.

18 Avo, mayo saa kamba ino nogala mvula ng'hulu ya mabwe nayo hainalawilila mwiisi ya Misili toka mwanduso wake mbaka lelo.

19 Avo lagiza fugo zako zose na kila kinhu kili mmigunda kikigwe goya kwavija mvula ya mabwe yomtowela kila munhu na kila mnyama yeli kumgunda hebu kunze ya ng'anda na wose wofa.’ ”

20 Lakini watawala wa Falao wadumbile gaja gayalongile Mndewa Imulungu walopola wawasegesa watumwa zao na wanyama zao mmigunda wawagala mzing'anda.

21 Lakini waja hawagagelegeze gaja gayalongile Mndewa Imulungu wazileka fugo zao na watumwa zao mmiguda.

22 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela Musa, “Golosa mkono wako uchanha kuulanga, ili mvula ya mabwe itowe kila hanhu mwiisi ya

Misili, kwa kila munhu na kila mnyama na kila kinhu kili mmigunda."

23 Musa viyaugolose mkono wake uchanha kuulanga, Mndewa Imulungu kagala mvula ya mabwe na ng'huwa na mimwesa mwiisi. Avo Mndewa Imulungu kagala mvula ya mabwe kila hanhu mwiisi ya Misili.

24 Mvula ng'hulu ya mabwe na mimwesa igendelela kutowa, kuduhu mwenekae yoyose wa Misili yawahile kuchona kinhu kamba acho.

25 Mvula ya mabwe itowa kila hanhu mwiisi ya Misili na ibananga migunda yose. Mvula ayo iwakoma wanyama wose na wanhu wose wakalile kunze, ibena vinhu vose vihandigwe mmigunda na mibiki.

26 Lakini mvula ya mabwe haitowile mwambu wa Gosheni, kuko kuwakalile okala Waizilaeli.

27 Falao kalagiza Musa na Haluni wakemigwe, kawalongela, "Mwanza uno nitenda nzambi, Mndewa Imulungu katenda goya, niye na wanhu zangu tubananga.

28 Mpuleni Mndewa Imulungu! Kwavija ng'huwa zino na mvula ino vibanza, niye nowaleka musegele na honda mukawe kusegela."

29 Musa kamwidika Falao, "Sambi baha nahasegela kudibuga dino, noigolosa mikono yangu nompula Mndewa Imulungu, mvula na ng'huwa voleka, na kokuwa kuduhu mvula ya mabwe, baho gweye kojuwa isi yose ya Mndewa Imulungu.

30 Lakini nojuwa gweye na watawala zako hamumdumba bule Mndewa Imulungu."

31 Minoga ya kutendela viwalo va kitani na
shayili vose vikala vinangigwe, kwavija shayili
ikala yosonga kunamiza na minoga ya kutendela
viwalo va kitani ikala yokwalika.
32 Lakini ngano na minoga iyagwe iigalile na
ngano havinangigwe kwavija vikawaga kukan-
gala.

33 Avo Musa kasegela kwa Falao, kachola kunze
kudibuga, kagolosa makono gake kampula Mn-
dewa Imulungu. Ng'huwa na mvula ya mabwe
vileka kutowa.
34 Falao viyonile mvula ya mabwe na ng'huwa
vileka kutowa, katenda nzambi kabili, heyo na
watawala zake watenda mizoyo yao iwe midala.
35 Avo, kalema kuwaleka Waizilaeli wasegele,
kamba Mndewa Imulungu viyalongile kwa mu-
lomo wa Musa.

# 10

### *Mbalangulu*

1 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela Musa,
“Genda kwa Falao, kwavija niye niwatenda heyo
na watawala zake wawe na mizoyo midala ili
nitende unzonza hagati yao.
2 Avo, mweye muwasimulile wanenu na
wazukulu zenu, viniwagelile bumbuwazi
Wamisili kwa kutenda vilaguso hagati yao, na
baho mweye mojuwa kamba niye na Mndewa
Imulungu.”

3 Avo Musa na Haluni wachola kwa Falao wa-
mulongela, “Mndewa Imulungu wa Waebulania

kolonga, ‘Mbaka lini kolema kugwa kinguban-
guba kuulongozi wangu? Waleke wanhu zangu
wasegele, wakanitambikile.

4 Wahalema kuwaleka wanhu zangu wasegele,
mayo nogala mbalangulu mwiisi yako.

5 Isi yose yogubikigwa na mbalangulu na
kuduhu hanhu honda honeke. Na woja kila
kinhu kidodo kisigasigwe na mvula ya mabwe,
vivija woja hata mibiki isigale.

6 Mbalangulu wao omema mzing'anda zako
na mzing'anda za watawala zako na ng'anda za
Wamisili wose. Okuwa wengi hata wahenga zenu
hawanachona kinhu kamba acho toka viwaleleke
mbaka lelo.’ ” Abaho Musa kasegela kwa Falao.

7 Watawala wa Falao wamuuza, “Vino,
munhu ino kotugaza mbaka lini? Waleke
Waizilaeli wasegele, wakamtambikile Mndewa
Imulungu wao. Vino hulola kamba isi ya Misili
yobanangika?”

8 Abaho Musa na Haluni wakemigwa wabwele-
ganye kwa Falao, nayo Falao kawalongela, “Gen-
deni mkamtambikile Mndewa Imulungu wenu.
Lakini nouza, kina nani onda wachole hamoja na
mweye?”

9 Musa kamwidika, “Tochola hamoja na wab-
wanga na wavele na wanetu wa kimbigalo na
wa kitwanzi, ng'hondolo na ng'ombe na mbuzi,
kwavija tolondigwa tukamtendele nyimwiliny-
imwili Mndewa Imulungu.”

10 Lakini Falao kawalongela, “Mawe! Mndewa
Imulungu yawe hamoja na mweye, kamba na-
hawatogolela mweye mugende, hamoja na wat-

wanzi na wanenu! Niye nokona mweye mo-
gelegeza gehile mmizoyo yenu.
11 Bule! Wambigalo waiyeka wao onda wac-
hole kumtambikila Mndewa Imulungu, kwavija
mbuli ayo iyo imulonda.” Abaho Musa na Haluni
wawingigwa kuulongozi wa Falao.

12 Mndewa Imulungu kamulongela Musa,
“Golosa fimbo yako uchanha mwiisi ya Misili,
ili mbalangulu walawilile na wengile mmigunda
na waje minoga yose ili mmigunda, na kila kinhu
kilekigwe kunangigwa na mvula ya mabwe.”
13 Avo Musa kagolosa fimbo yake uchanha mwi-
isi ya Misili. Mndewa Imulungu kagala beho ku-
lawa mwambu wa kudilawilila zuwa na beho dijo
dibuma uchanha mwiisi, imisi mbaka kilo chose.
Imitondo beho dijo digala mbalangulu.
14 Mbalangulu awo wenela kila hanhu mwiisi
ya Misili, wahumulukila uchanha mwiisi yose.
Mbalangulu awo wakala madali kwa madali.
Hawanalawilila mbalangulu kamba wano na
honda walawilile kabili.
15 Waigubika isi yose ya Misili mbaka ikala
ziza. Wakija kila kinhu kisigasigwe na mvula
ya mabwe na waija minoga na matunda gakalile
mna imigunda. Kuduhu tepo jojose disigale
mdibiki wala mna iminoga mwiisi ya Misili.

16 Abaho Falao kalopola kawakema Musa na
Haluni, kawalongela, “Niye nibananga kwa Mn-
dewa Imulungu wenu, na kumwenu mweye.
17 Avo nowapula mugele kumgongo nzambi
zangu mwanza uno na Mndewa Imulungu wenu
yanisegesele mbuli ino igala ifa.”

18 Musa kasegela kwa Falao na kachola
kumpula Mndewa Imulungu.
19 Nayo Mndewa Imulungu kagala beho kulu
kulawa mwambu wa kudihongela zuwa diwap-
wililisa mbalangulu wose na diwagala mbahali ya
Shamu. Kuduhu hata mbalangulu yasigale mwiisi
ya Misili.
20 Lakini Mndewa Imulungu kamtenda Falao
yawe na moyo mdala, nayo hawalekile Waizilaeli
wasegele.

### *Ziza*

21 Abaho Mndewa Imulungu kamulongela
Musa, "Golosa mkono wako uchanha kuulanga,
isi ya Misili iwe na ziza, wanhu wababase babase
mdiziza."
22 Avo Musa kagolosa mkono wake uchanha
kuulanga, kukala na ziza totolo mwiisi yose ya
Misili kwa siku ndatu.
23 Kuduhu munhu yadahile kumona miyage
hebu munhu kusegela hanhu hayakalile kwa siku
ndatu. Lakini Waizilaeli wose hanhu hawakalile
kukala na mulenge.
24 Abaho Falao kamkema Musa kamulongela,
"Gendeni mkamtambikile Mndewa Imulungu.
Watwanzi na wanenu vivija odaha kuchola
hamoja na mweye. Lakini ng'hondolo zenu na
ng'ombe na mbuzi osigala."
25 Lakini Musa kamulongela, "Wahatenda vivo
gweye utugwelele wanyama wa nhosa na nhosa
ya kusoma moto ili tukamtambikile Mndewa Imu-
lungu wetu.
26 Tolondigwa tuwasole wanyama wetu wala
kuduhu hata imoja yonda yasigale. Kwavija

kwa iwanyama awo tomulavila nhosa Mndewa Imulungu wetu, na mbaka sambi siye hatujuwa mbaka twahavika kuko, kinhu gani tolondigwa tukamulavile nhosa Mndewa."
27 Lakini Mndewa Imulungu kamtenda Falao yawe na moyo mdala na kalema kuwaleka Waizilaeli wasegele.
28 Falao kamulongela Musa, "Segela, witeganye sikuuchone kihanga changu kabili, kwavija siku yonda uchone kihanga changu kofa!"
29 Musa kamwidika, "Kulonga goya, sichona kabili kihanga chako."

# 11

## *Ifa ya wana wa chaudele wa Wamisili*

1 Mndewa Imulungu kamulongela Musa, "Ding'hali kubulo dimoja disigala nomtowa najo Falao na Wamisili, abaho kumwande kowalekeseni musegele hano, na heyo mwenyego kowawinga musegele mwiisi yake.
2 Walongele Waizilaeli kamba kila mbigalo na mtwanzi yampule munhu wa behi yake vinhu va shaba na zahabu."
3 Mndewa Imulungu kawatenda Waizilaeli wanogeligwe na Wamisili, na Musa mwenyego kawa munhu mkulu ng'hani mwiisi ya Misili, mgameso ga watawala wa Falao hamoja na wanhu wose.
4 Musa kamulongela Falao, "Mndewa Imulungu kolonga vino, 'Kilo kikulu, lelo nobita hagati ya isi ya Misili.
5 Nahabita kila chaudele wa kimbigalo mwiisi ya Misili kofa. Kusongela chaudele wako gweye

Falao ija yeli muhazi wako mbaka chaudele wa
msang'hanaji wako ija yoduga kwa dibwe. Hata
chaudele wa fugo zako vivija wofa.
6 Hokuwa na kililo kikulu mwiisi yose ya Misili,
kililo acho hakinalawilila, na honda kilawilile ka-
bili.
7 Lakini mna iwanhu wa Izilaeli kokuwa
kuduhu kililo na kokuwa na tindiwalo,
baho kojuwa kamba Mndewa Imulungu ayo
yowabagula Waizilaeli na Wamisili.' ”
8 Abaho Musa kamulongela Falao,
“Wasang'hanaji zako okwiza kumwangu na
kunifugamila na onipula nisegele mwiisi ya Misili
niye na wanhu wose onikweleleza. Gahamala
gago nosegela.” Abaho Musa kasegela kwa Falao
kuno kagevuzika.
9 Mndewa Imulungu kamulongela Musa, “Falao
honda yakutegeleze ili nhende ng'hani unzonza
mwiisi ya Misili.”
10 Avo Musa na Haluni watenda unzonza wose
mgameso ga Falao. Lakini Mndewa Imulungu
kamtenda Falao yawe na moyo mdala, kalema
kuwaleka Waizilaeli wasegele mwiisi yake.

# 12

*Pasaka*

1 Viwakalile wang'hali mwiisi ya Misili, Mn-
dewa Imulungu kamulongela Musa na Haluni,
2 “Mwezi uno okuwa mwezi wa ichanduso wa
mwaka kumwenu.
3 Walongele Waizilaeli kamba mdisiku da longo
da mwezi uno, kila munhu mng'anda yake yasole
mwana ng'hondolo, hebu mwana mbuzi.

4 Kamba ng'anda ina wanhu wadodo na
haidaha kumuja mwana ng'hondolo wose,
iilumbe na wayao weli behi nao wamuje kamba
hewo viweli, na wasagule mnyama yodaha
kugoligwa kwa kila munhu kamba viyodaha
kuja.
5 Mnyama ayo yonda mumsagule yatelele,
na yawe mbigalo na yawe wa mwaka umoja
na modaha kumsola mwana ng'hondolo hebu
mwana mbuzi.
6 Kila ng'anda imkalize mbaka siku da longo na
nne ya mwezi uno, wanhu wa Izilaeli olondigwa
wawachinje wanyama awo ichungulo.
7 Abaho wasole idamu ya wanyama awo
na kuibaka mna iviwambaza va imilango na
uchanha ya imilango, mumo monda wadile
izinyama.
8 Kilo acho nyama ayo ibanikigwe na idigwe
hamoja na kinhu kili usungu na gate hadigeligwe
hamila.
9 Sikuidigwe ing'hali mbisi hebu
